

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



MKUU WA TAKUKURU MKOA
Mtaa wa Uzunguni,
S.L.P 37,
37101 SHINYANGA,
Tanzania.
Simu: (028) 2762630
Nukushi: (028) 2763358

01 Julai 2020.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAKUKURU SHINYANGA YAFUNGUA KESI TATU (3) MAHAKAMANI MWEZI JUNI NA INAMSHIKILIA ASHA MWANDU MAKWAIYA AMBAYE MJUMBE WA CCM MKUTANO MKUU TAIFA KWA KOSA LA KUTOA RUSHWA KWA WAJUMBE WA (UWT).

Tarehe 30.06.2020 **TAKUKURU** Shinyanga imefungua kesi namba CC.NA.8/2020 mbele ya Mh. Masesa, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Shinyanga dhidi ya Machiya Mhela Kashije (Mhasibu Kamati ya Fedha za walengwa TASAF) na Jisabo Dioniz Jidamabi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha za walengwa TASAF) kwa kosa la kupokea fedha za Rushwa za walengwa wa TASAF wa Kijiji cha Negezi kinyume cha sheria wakati wao si walegwa kiasi cha sh. 159,000/= kwa madai kuwa watawapelekea fedha hizo kitu ambacho siyo kweli na kinyume na Kf 15(1)(a) na 15(2) cha sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa, washtakiwa hao walikiri kutenda kosa hilo.

Mhe. Masesa, Hakimu Mkazi wa Shinyanga alisoma hukumu mbele ya Mwendesha Mashtaka wa **TAKUKURU** Sengoka Mndambi ambapo Machiya Mhela Kashije na Jisabo Dioniz Jidamabi walipatikana na hatia ya kutenda kosa la kupokea rushwa hivyo Mahakama imewataka kwenda jela mwaka mmoja kila mmoja au kulipa faini ya shs 500,000.00 kwa kila mmoja.

Tarehe 30.06.2020 **TAKUKURU** Shinyanga imefungua kesi CC.NA.117/2020 mbele ya Mh. J.P. Rwehabula, Hakimu mfawidhi Mahakama ya Wilaya Kishapu Shinyanga dhidi ya Julius Lwenya Jidayi na Deus Jilungu Jipoya. Julius Lwenya Jidayi akiwa mwenyekiti wa kijiji cha Igaga B aliomba kiasi cha sh. 20,000/= kutoka kwa Kashinje Bili Shagembe kama hongo kutoka kwa Kashinje Bili Shagembe, ili aweze kuandaa barua ya utambulisho ya malalamiko kwenda kituo cha polisi Kishapu. Deus Jilungu Jipoya ambaye ni Mtendaji wa Kijiji cha Igaga B alipokea kiasi hicho cha sh. 20,000/= kutoka kwa Kashinje Bili Shagembe kitendo ambacho ni kosa kwa mujibu wa kf 15 cha Sheria ya Kuzuia na kupambana Rushwa. Washtakiwa walikana kosa, wako nje kwa dhamana na kesi imepangwa kusikilizwa tarehe 14/07/2020.

Tarehe 26.06.2020 **TAKUKURU** Shinyanga imefungua kesi CC.NA.116/2020 mbele ya Mh. J.P. Rwehabula, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kishapu dhidi ya Joseph Charles Luponya akiwa kama Kaimu Mkuu wa shule ya msingi Bupigi alipokea kiasi cha Tsh. 400,000/= kutoka kwa Mwigulu Nalija Shalali ambaye ni mzazi wa Gambi Mwigulu Nalija anayejulikana pia kwa jina la **JUMA** ili asiweze kuchukua hatua za kisheria juu ya kijana aitwaye Gambi Mwigulu Nalija aliyekuwa anatuhumiwa kwa kosa la kubaka mwanafunzi wa darasa la tano (5) aitwaye Yunis Mahona Dotto. Shauri limehairishwa mpaka tarehe 21/07/2020 Litakapoendelea na usikilizwaji.

Tarehe 28/06/2020 **TAKUKURU** mkoa wa Shinyanga katika ufuatiliaji wa vitendo vya Rushwa kuelekea kipindi hiki cha uchaguzi ilimkamata Bi Asha Mwandu Makwaiya ambaye ni mkazi wa Majengo Mapya - Shinyanga mjini na mjumbe wa CCM mkutano Mkuu Taifa akiwa nyumbani kwa Elithabeth Donald Itete (Mama Buzwizwi) ambaye ni Katibu wa UWT Tawi la Mshikamano pamoja na wajumbe wengine (10) ambao ni viongozi wa (UWT) kata ya Ngokoro. Bi Asha Mwandu Makwaiya alitaka kugawa mashuka (10), kitenge (1) na ndala (11) kwa wajumbe (11) wa Umoja wa Jumuiya ya Wanawake CCM (UWT) kata ya Ngokoro kama kishawishi cha yeye kuchaguliwa au kuchaguliwa kwa aliyemtuma.

WITO

Wananchi wote wa mkoa wa Shinyanga waendeleo kutoa ushirikiano kwa **TAKUKURU** kama ambavyo wamekuwa wakifanya, ili kuhakikisha kuwa tunaondoa kero ya rushwa katika mkoa wetu hasa katika kipindi hiki tunachoelekea kuanza michakato ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi Mkuu mwaka huu 2020.

Imetolewa na H.M.Mussa Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.